

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

Tele: +255 026 2322761-5  
Fax No. +255 026 2324218  
E-mail: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)



Ofisiya Bunge  
S.L.P. 941  
**DODOMA.**

### TAARIFA KWA UMMA

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 6 wa Mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Act, 2019*) umesomwa Bungeni kwa mara ya Kwanza tarehe 4 Septemba, 2019 ambapo mara baada ya hapo Mheshimiwa Spika ameupeleka katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Sheria Ndogo imepanga kusikiliza maoni ya wadau kuhusu Muswada huo siku ya Ijumaa tarehe 6 Septemba, 2019 kuanzia saa 7:00 mchana na siku ya Jumamosi tarehe 7 Septemba, 2019 kuanzia saa 4:00 asubuhi katika ukumbi Na. 9 Jengo la Utawala – Ofisi za Bunge, Dodoma.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huo, Kamati inawaalika wadau wote kufika na kuwasilisha maoni yao kabla Muswada huo haujapelekwa katika hatua nyingine. Maoni ya wadau pia yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya posta au Barua pepe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu wa Bunge,  
Ofisi ya Bunge,  
S.L.P 941,  
**DODOMA.**

Barua pepe: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)

Muswada huo pia unaweza kupakuliwa kupitia tovuti ya [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz)

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,  
Ofisi ya Bunge,  
S.L.P 941,  
**DODOMA.**

05 Septemba, 2019.